

Mpango wa Infant-Toddler (Watoto Wachanga na Wadogo) wa North Carolina

ARIFA YA MFUMO WA MALIPO

Shirika lillo katika mstari wa mbele kwenye Mpango wa Infant-Toddler wa North Carolina Early Intervention Branch of the Women's and Children's Health Section katika NC Division of Public Health. Katika ngazi ya eneo, Mashirika ya Huduma za Ukuzaji wa Watoto (CDSAs) husimamia shughuli za ITP. Notisi hii iliyoandikwa ni ya kukuarifu kuhusu Mfumo wa Malipo wa ITP. Hati hii ni muhtasari wa Sera ya Ada, Bili na Kurejeshewa pesa ya ITP na maelezo mengine husika ambayo yanaweza kupatikana kwa ukaguzi katika tovuti ya Mpango, www.beeearly.nc.gov, Sehemu ya Nyenzo / Machapisho.

MIZANI MAALUM YA KUBAINI UWEZO WA KULIPA (SFS) YA ITP:

- ITP hutumia Mizani Maalum ya Kubaini Uwezo wa Kulipa (SFS) kubaini uwezo au kutoweza kwa familia kulipia huduma za ITP.
- Unaweza kupata nakala ya SFS ya ITP na Ratiba za Ada kwenye tovuti ya Mpango (www.beeearly.nc.gov).
- Hakuna familia inayoweza kunyimwa huduma za ITP kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kulipa.

HUDUMA "ZISIZOLIPISHWA ZA FAMILIA":

- Huduma zifuatazo za ITP zinatolewa bila malipo kwa familia zote, bila kujali uwezo uliobainishwa wa familia wa kulipa:
 - shughuli za kutafuta mtoto, tathmini, uratibu wa huduma, shughuli za utawala na uratibu zinazohusiana na kubuni, ukaguzi na tathmini ya Mpango wa Familia wa Huduma Iliyobinafsishwa (IFSP) na utekelezaji wa ulinzi wa utaratibu.
- Huduma zote zinazotolewa kwa familia kabla ya Matayarisho ya Awali ya IFSP (uandikishaji) ni Huduma za "Zisizolipishwa za Familia".

HUDUMA "ZINAZOWEZA KUTOZWA":

- "Huduma Zinazoweza Kutozwa" ni huduma nyingine zote za ITP, isipokuwa zile zilizoordheshwa hapo juu kama Huduma "Zisizolipishwa za Familia".
- Mgao wa familia (asilimia ya SFS) hutumika kwa huduma zote za ITP zinazotozwa, zilizoidhinishwa na familia, kwenye IFSP.

UTHIBITISHAJI WA MAPATO / UBAINISHAJI WA SFS:

- Ukubwa wa familia na mapato ya jumla yaliyorekebishwa ya familia hutumiwa kubainisha asilimia ya SFS au mgao wa familia.
- Hati za uthibitishaji huombwa wakati wa uelekezaji na kila mwaka baada ya kujiandikisha.
- Ikiwa familia imebainishwa kuwa haiwezi kulipia huduma za ITP, SFS% itawekwa kuwa 0%.
- Ikiwa familia itakataa kutoa maelezo yanayohitajika ya ukubwa wa familia na uthibitishaji wa mapato, asilimia yao ya SFS itawekwa kwa 100%.
- Familia itaarifiwa kuhusu SFS% yao na wafanyakazi wa CDSA ili kuzingatia gharama ya huduma za IFSP wakati wa kuchagua kukubali au kukataa huduma.
- Kama inavyofanuliwa kwenye *Notisi ya Haki ya Watoto na Familia ya Mpango wa North Carolina Infant-Toddler*, familia inaweza kupinga kuwekwa kwa ada yoyote wakati wowote.
- Upeo wa Kila Mwezi - Mgao wa gharama ya kila mwezi ya familia kwa huduma zinazopingwa kwenye IFSP haipaswi kuzidi 5% ya mapato ya kila mwezi ya familia. CDSA itaarifu familia kuhusu kiasi chao cha kila mwezi.

MAREKEBISHO YA MALIPO YA KUISHI KATIKA HALI NGUMU:

- Familia inaweza kutuma maombi wakati wowote kwa ajili ya kuzingatia marekebisho ya malipo ya kuishi katika hali ngumu kwa asilimia yao ya SFS ikiwa hali yao ya kifedha itabadilika au itaathiriwa na gharama zozote za matibabu zisizo za kawaida.

IDHINI YA MATUMIZI YA BIMA YA BINAFSI NA MEDICAID:

- Huduma za "Zisizolipishwa Familia" - Kwa idhini iliyoandikwa, ITP itatoza bima ya kibinafsi na/au bima ya umma (Medicaid) kwa huduma hizi. Iwapo idhini ya bili hakijatolewa, ITP lazima bado itoe huduma zisizolipishwa familia, ambazo mzazi ametoa idhini kupokea, bila kuchelewa au kunyimwa na bila gharama yoyote kwa familia.
- Huduma Zinazotozwa - Kupitia idhini iliyoandikwa kutoka kwa familia ya kulipia bima ya binafsi na/au bima ya umma (Medicaid), ITP itatoza vyanzo hivi kwa huduma za ITP:
 - Wakati huduma ya ITP hailindwi na mpango wa faida ya bima, mgao wa gharama kwa familia (asilimia ya SFS) utatozwa kwenye Kiwango cha ITP (Kiwango cha Medicaid) kwa huduma zinazotozwa.
 - Wakati huduma ya ITP inalindwa na bima, mgao wa gharama kwa familia (asilimia ya SFS) itatozwa kwa mpango wowote wa bima uliokabidhiwa salio baada ya malipo ya faida ya mpango kufanywa. Familia haitatozwa kiasi kinachozidi kiwango cha ITP (kiwango cha Medicaid).

MEDICAID:

- ITP haiwezi kuhitaji mtoto aandikishwe katika Medicaid ili apokee huduma za ITP.
- Ikiwa mtoto ameandikishwa katika Medicaid, sharti mzazi atoe idhini kabla ya hatua ambayo mtoa huduma wa ITP atafichua maelezo ya binafsi yanayomtambulisha kwa Medicaid kwa madhumuni ya utozaji.
- Mzazi ana haki ya kuondoa idhini ya kufichua maelezo yanayomtambulisha mtu binafsi kwa Medicaid kwa madhumuni ya utozaji.
- Matumizi ya Medicaid kwa Huduma za Uingiliaji wa Mapema North Carolina HAYASABABISHI hali yoyote kati ya zifuatazo:
 - 1) Kupungua kwa bima inayopatikana ya maisha au manufaa yoyote ya bima kwa ajili ya mtoto au mzazi huyo chini ya mpango huo,
 - 2) Wazazi wa mtoto kulipia huduma ambazo zingegharamiwa na manufaa ya umma au mpango wa bima,
 - 3) Kuongezeka kwa malipo au kusitishwa kwa manufaa ya umma au bima kwa mtoto au mzazi, au
 - 4) Kutostahiki kwa mtoto au wazazi wa mtoto kwa msamaha wa nyumbani na wa jumuiya kulingana na jumla ya gharama inayohusiana na afya.
- Ikiwa mtoto analindwa na bima ya umma (Medicaid) na bima ya binafsi, sera ya Medicaid inahitaji kwamba bima ya binafsi ilipwe kwanza. Ikiwa bima ya binafsi itatozwa, kampuni ya bima inaweza kutuma Ufafanuzi wa Manufaa (EOB) na malipo kwa familia badala kuzituma moja kwa moja kwa mtoa huduma. Familia ikipokea malipo, hundi na karatasi zote lazima zikabidhiwe kwa mtoa huduma wa ITP kwa ajili ya malipo.

BIMA YA KIBINAFSI:

- Sharti mzazi atoe idhini ya kuandikwa ili ITP itumie bima ya kibinafsi kulipia huduma za uingiliaji mapema za mtoto. Huenda kukawa na gharama zinazohusiana na kutoza bima ya kibinafsi kwa huduma za ITP. Mifano ya mpango wa bima uliogawiwa salio ambazo familia inaweza kuwajibika kwayo ni ugavi wa malipo, bonasi, matozo na bima.
- Mzazi ana chaguo la kuchagua kutotoza bima ya kibinafsi na kulipia moja kwa moja huduma zinazotozwa kwa kiwango cha ITP (kiwango cha Medicaid).
- Ikiwa mzazi atachagua kutoa idhini ya kutumia bima ya kibinafsi kulipia huduma za ITP:
 - Sharti mzazi atoe idhini ya kuandikwa kabla ITP itumie bima ya kibinafsi kulipia huduma za uingiliaji mapema za mtoto.
 - Idhini iliyoandikwa ya mzazi inahitajika wakati wowote kunapokuwa na ongezeko (kujirudia, muda, au kiasi) katika utoaji wa huduma kwenye IFSP.
- Ikiwa bima itatozwa, kampuni ya bima inaweza kutuma Ufafanuzi wa Manufaa na malipo kwa familia badala kuzituma moja kwa moja kwa mtoa huduma. Hii ikitokea, hundi na karatasi zote lazima zikabidhiwe kwa mtoa huduma wa ITP kwa ajili ya malipo.

SERA YA UKUSANYAJI ADA YA CDSA:

Malipo yote ya huduma zinazotolewa na CDSA na watoa huduma wa ITP walioidhinishwa yanapaswa kulipwa ndani ya siku 30 kutoka tarehe ya ankara na familia zinatarajiwa kulipa ndani ya kipindi hiki cha muda. Ikiwa malipo hayatafanywa kwa miezi mitatu kutoka kwa ankara ya awali bila mipango ya mpango wa malipo, CDSA ina wajibu wa kuanzisha taratibu za kukusanya. Hii ni pamoja na 1) kuarifu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa North Carolina kuhusu akaunti iliyo na deni ambayo muda wake ulipita, na 2) CDSA ina wajibu wa kuwasilisha akaunti zenye deni zisizolipwa kwa Idara ya Mapato ya North Carolina, chini ya Ukusanyaji wa Madeni Dhidi ya Sera ya Kurejesha Pesa za Kodi ya Mapato ya Mtu Binafsi kwa mujibu wa GS. 105A Sheria ya Ukusanyaji wa Deni. Hii ina maana kwamba fedha kutoka kwa marejesho ya kodi ya mtu binafsi zinaweza kuziwa dhidi ya deni lolote ambalo halijalipwa kwa CDSA kwa huduma zinazotolewa.

SABABU YA ITP KUOMBA NAMBARI YA USALAMA WA JAMII:

ITP imejitahidi ili kupunguza matumizi ya Nambari ya Usalamawa Jamii katika shughuli zake. ITP inapaswa kuomba Nambari ya Usalama wa Jamii ya mtu mzima ambaye anawajibikia kifedha mtoto anayeelekezwa au aliyesajiliwa katika ITP. ITP huomba Nambari ya Usalama wa Jamii ya mzazi ili kutimiza wajibu wake wa kisheria kwa Serikali chini ya N.C.G.S. 105A-3 na N.C.G.S. 147-86.21 kukiwa na haja ya kukusanya deni ambalo linadaiwa na Shirika hili. Sheria ya Jimbo na Serikali inalinda faragha na usalama wa Nambari za Usalama wa Jamii na ITP haitafichua Nambari za Usalama wa Jamii kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kukusanya deni, au vinginevyo inavyotakiwa na sheria.

SERA YA FARAGHA

Sheria ya Family Education Rights and Privacy (FERPA)

Sheria ya Family Education Rights and Privacy (FERPA) ni sheria ya jimbo ambayo inalinda faragha ya watoto na wazazi wanaopokea huduma kutoka kwa ITP. Maelezo kuhusu mtoto au mwanafamilia ni ya siri na hayapaswi kutumwa kati ya watoa huduma bila idhini ya kuandikwa kutoka kwa mzazi, isipokuwa katika hali maalum ambapo kutolewa huku kunaruhusiwa na sheria kama vile dharura ya afya au usalama, chini ya agizo la mahakama, au kama shughuli ya kupata mtoto inaruhusiwa. Hata hivyo, shirika, linaweza kutoa maelezo ya siri kwa wafanyakazi wake ambao wana idhini ya ufikiaji wa maelezo.

Maswali Yanayoulizwa Sana

Gharama za Huduma za Mpango wa Infant-Toddler (ITP)

- 1. Je, itagharimu familia yangu nini kushiriki katika Mpango wa Infant-Toddler? Mgao wangu wa gharama utabainishwa vipi?**
Baadhi ya familia zinaweza kushiriki katika gharama ya huduma za uingiliaji mapema kulingana na kiwango cha ada (SFS) ambayo inazingatia mapato ya jumla yaliyorekebisha (AGI) na ukubwa wa familia. Asilimia ya kiwango cha ada huweka uwezo wa familia kulipa au kushiriki gharama. Asilimia ya kiwango cha kiwango cha ada itabainishwa kabla ya mtoto kujiandikisha katika ITP na inakaguliwa kila mwaka.
- 2. Ninahitaji kutoa maelezo gani ili kuamua mgao wangu wa gharama?**
Utahitaji kutoa maelezo kuhusu familia yako kwa mratibu wako wa huduma. Hii inajumuisha wote wanaoishi katika kaya yako, umri wao, na jinsi wewe na mtoto wako mnavyohusiana nao. Ni lazima pia uwasilishe hati za kifedha kwa ofisi ya biashara kwenye ofisi ya rasmi Children's Developmental Services Agency (CDSA) ili kuthibitisha AGI ya familia yako. Kuthibitisha uandikishaji katika mpango mwingine wa serikali, kama vile Medicaid, kunaweza kutosha kuweka asilimia yako ya SFS. Kwenye fomu ya *Arifa ya Uthibitishaji wa Mapato ya Mpango wa North Carolina Infant-Toddler*, utapata maelezo kuhusu hati zinazohitajika ili kuthibitisha mapato yako, muda unaohitajika na anwani ya mawasiliano ya ofisi ya kazi ya CDSA. Kuchagua kutowasilisha hati za kifedha hufanya asilimia yako ya SFS kuwa 100%. Hiyo inamaanisha kuwa utawajibika kulipia huduma zote zinazotowazwa.
- 3. Je, kuna ada unazotowazwa kupokea huduma za Mpango wa Infant-Toddler?**
Huduma nyingi hutolea bila malipo kwa familia zote. Huduma hizi ambazo hazina gharama kwa familia ni shughuli za kutafuta watoto, uratibu wa huduma, tathmini, ukuzaji na ukaguzi wa Mpango wa Huduma ya Familia Iliyobinafsishwa (IFSP), na shughuli za kuhakikisha haki za familia. Familia zinaweza kulipia huduma nyingine zozote. Mratibu wako wa huduma atakagua kila huduma kwenye IFSP na kukuarifu ikiwa huduma inaweza kuwa na gharama kwa familia.
- 4. Bima yangu ya afya itatowazwa?**
Bima ya kibinafsi ya familia yako itatowazwa kwa huduma, kupitia idhini yako. Ukikubali, asilimia ya SFS itatumika kwa gharama zozote za msingi ambazo mpango wako wa bima utaipa familia. Hizi ni pamoja na ugavi wa malipo, bima na makato. Baadhi ya mipango ya bima ya afya hulipia huduma za uingiliaji mapema kulingana na manufaa ya bima ya mtoto wako. Ikiwa huduma hailindwi, malipo ya msingi ya huduma yatakuwa kiwango cha ITP (ambacho ni Kiwango cha Medicaid). Asilimia ya SFS itatumika kwenye ada msingi. Medicaid au vyanzo vingine vya ufadhili wa umma vitatowazwa ipasavyo, kwa idhini yako.
- 5. Je, na hali ya kifedha ya familia yangu ikibadilika baada ya ugavi wa gharama kuamuliwa?**
Familia yako ikikumbwa na tukio la ghafla kama vile kupoteza kazi au mapato au gharama nyingi za matibabu, unaweza kuomba ukaguzi wa kifedha na marekebisho ya hali ngumu kifedha. Mratibu wako wa huduma anaweza kukusaidia katika mchakato huu.